HOTUBA YA MHE. WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIAO MHE. PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA (MB) KATIKA UZINDUZI WA BODI YA WAKURUGENZI YA SHIRIKA LA RELI TANZANIA (TRC)

Ndugu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi;

Ndugu Katibu Mkuu – Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano – Sekta ya Uchukuzi;

Ndugu wajumbe wa Bodi;

Mkurugenzi Mkuu, Ndg. Masanja Kungu Kadogosa;

Menejimenti ya Shirika la Reli Tanzania (TRC);

Viongozi wa Vyama vya wafanyakazi TRAWU na TAMICO;

Wafanyakazi wa Shirika la Reli;

Waandishi wa Habari;

Mabibi na Mabwana.

Habarini za asubuhi.

Kabla ya kuanza shughuli yetu naomba nimshukuru M/Mungu kwa kutujalia kua hai na afya na tukaweza kukutana hapa leo hii kwa dhamira ya kuendeleza ujenzi wa Taifa letu. Pili ningependa kuwashukuru wajumbe pamoja na wageni wetu wote waalikwa mliohudhuria kwa kuacha shughuli zenu ama za ujenzi wa Taifa au za binafsi na kuja kujumuika nasi ili kuweza kufanikisha uzinduzi wa Bodi ya Wakurugenzi itakayofanya kazi bega kwa bega na Shirika la Reli, nasema asanteni na karibuni sana. Baada ya shukrani hizo naomba nitoe maelezo mafupi kuhusu azma ya kikao chetu hiki. Mjumuiko huu upo kwa nia ya kuzindua bodi ya Wakurugenzi ambapo wajumbe wake tayari wameshateuliwa na Bodi inatakiwa ianze shughuli zake haraka iwezekanavyo ili nasi tusionekane kuwa tupo nyuma ya wakati.

Ndugu Mwenyekiti, ndugu wajumbe na wageni waalikwa

Kama tunavyotambua, Shirika la Reli nchini limeanzishwa rasmi na Sheria ya Reli Na. 10 ya Mwaka 2017 baada ya kuunganisha Mashirika mawili ya Serikali yaani Shirika Hodhi la Rasilimali za Reli nchini (RAHCO) na Kampuni ya Reli (TRL). Ili kuongeza tija, Serikali iliona ni vyema makampuni haya yaungane ili yaweze kufanya kazi kwa pamoja na ukaribu Zaidi. Aidha, TRL imekuwa na Bodi ya Wakurugenzi wakati RAHCO kwa muda mrefu haikuwa na Bodi ya Wakurugenzi. Napenda kutambua kazi kubwa iliyofanywa na iliyokuwa Bodi ya TRL chini ya usimamizi wa Mwenyekiti wa Bodi, Eng. Kondoro kwa kuiwezesha TRL kukabiliana na Changamoto lukuki ambazo watumishi walikuwa nazo.

Ndugu Mwenyekiti, Ndugu Wajumbe na wageni waalikwa;

Dhamira ya kuundwa kwa Shirika la Reli nchini imepelekea kutungwa kwa Sheria ili Taasisi hiyo iweze kuwepo kwa mujibu wa Sheria, iwe na mamlaka,maamuzi na nguvu za kisheria wakati wa kutekeleza majukumu yake. Sheria ya Reli Na. 10 ya 2017 ilipitishwa na kutiwa saini na Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dr. John Joseph Pombe Magufuli na kuanza kutumika rasmi tarehe 29, Februari 2017. Sheria imetoa mamlaka kwa Waziri mwenye dhamana na Uchukuzi kutayarisha kanuni ambazo kwa sasa ziko kwenye hatua za mwisho kabla kuanza kutumika. Kutokana na Sheria hiyo ndio Bodi ya Wakurugenzi ikaundwa ili kusaidia utekelezaji wa kazi za Taasisi ya Reli ambayo nayo imeanzishwa chini ya Kifungu 11(1) cha Sheria hiyo.

Ndugu Mwenyekiti, Ndugu Wajumbe na wageni waalikwa;

Kwa mujibu wa sheria ya Reli, Bodi ya Wakurugenzi inaundwa na Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais ambaye ana uelewa wa masuala ya reli, wajumbe saba watakaoteuliwa na Waziri ambao wana utaalamu wa masuala ya Uhandisi, biashara, uchumi, sheria na masuala ya utumishi. Bodi hii, imezingatia matakwa ya kisheria na sasa kama muonavyo, wajumbe wa Bodi hii wametoka katika taasisi zenye ujuzi na utalaam wa maeneo haya. Aidha, wamebobea hasa

katika taaluma zao ambazo ni muhimu katika kusimamia sekta hii muhimu. Naomba kutoa tamko mbele yenu kwamba Uteuzi wa Mheshimiwa Rais kwa Mwenyekiti na Uteuzi wa Waziri kwa wajumbe wa Bodi umefanywa kwa vigezo vyote hivyo, lakini kubwa Zaidi ni Imani kubwa kwenu kuwaamini kwamba hamtoniangusha mtafanya yale tuliyotarajia. Sheria hiyo pamoja na kumpa mamlaka Waziri ya kuteua watu hao vigezo vya elimu na uzoefu vime zingatiwa. Ni imani yangu kwamba walioteuliwa wanavyo vigezo vinavyohitajika na watatekeleza majukumu ipasavyo.

Bodi ya wakurugenzi ndio muhimili mkuu wa Taasisi ya kusimamia uendelezaji wa sekta ndogo ya reli ambapo serikali inaipa kipaumbele kikubwa katika serikali ya awamu ya Tano kama ilivyoelezewa katika Ilani ya Chama Tawala, hili si jukumu dogo hivyo hamna budi kujivunia kuwa kati ya wajumbe wa kwanza wa Bodi ya TRC mpya yenye kazi kubwa na nzito ya kuwaletea wananchi reli ya Standard gauge itakayokuwa na treni za umeme za mwendokasi na kwa msingi huo ndugu wajumbe, mliopewa dhamana ya Bodi mnatakiwa mjitahidi kufanya kazi zenu kwa umahiri na umakini mkubwa ili kuhakikisha Taasisi inafikia lengo la Serikali la kuwa na shirika madhubuti la reli nchini.

Ndugu Mwenyekiti, Ndugu Wajumbe na wageni waalikwa;

Kazi nyengine kubwa ya Bodi ni kuajiri Wakuu wa Idara za Taasisi na wafanyakazi wengine kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo ambao watafanya kazi kwenye Shirika hili jipya la reli. Ndugu wajumbe hili ni jukumu zito linalohitaji umakini lakini uwepo wenu kama wajumbe wa Bodi unanipa Matumaini na faraja kwamba kazi hiyo mtaifanya kwa umakini, umahiri na uadilifu mkubwa. Naomba niwatanabahishe kwamba muundo pia wa Shirika hili jipya utaidhinishwa na Bodi hii, nikuombeni sana musaidie kuijenga taasisi yetu ambayo ni changa kwa muundo thabiti utakaowezesha Taasisi kufanya kazi zake kwa ufanisi na kua na hadhi ya kutambuliwa kimataifa.

Naomba pia nitanabahishe kwamba bila fedha hakuna ufanisi mzuri wa kazi na suala la fedha kwa Taasisi linatakiwa kuidhinishwa na Bodi. Kwa ujumla Sheria iliyounda Bodi ambayo ni Sheria No.10 ya 2017 inatoa mamlaka makubwa na mazito kwa Bodi na niwaombe muyabebe majukumu hayo kwa magego bila kuchoka au kukata tamaa.

Ndugu Mwenyekiti, Ndugu Wajumbe na wageni waalikwa;

Bodi hii itakua na uwezo wa kuunda kamati ndogo ndogo za kusaidia utekelezaji wa sheria pamoja na kanuni zake na kuhakikisha kwamba lengo la kuendeleza miundombinu ya reli na kusimamia usafirishaji wa abiria na mizigo linatimia. Ni imani yangu kwamba chini ya Mwenyekiti wa Bodi ambaye ni Mwanasayansi na mbobezi wa masuala ya reli kwa kipindi alichosimamia TRL nina imani kuwa kazi hizo zitafanywa kwa umakini na ustadi mkubwa sana. Uwepo wa Bodi hii utapelekea kuongezeka kwa usafirishaji wa bidhaa na abiria wenye ufanisi na ubora jambo ambalo litatuletea hadhi ya nchi yetu pamoja na kukuza uchumi wetu.

Mwenyekiti, Ndugu Wajumbe na wageni waalikwa;

Naomba nikutanabahisheni kwa mara nyingine tena kwamba kazi mliyokabidhiwa na Serikali ni kubwa na nyeti sana ambayo inagusa maisha ya watu kwa upande mmoja na mustakabali wa uchumi wa nchi yetu kwa upande wa pili. Niwaombeni mfanye kazi zenu kwa kujiamini na kuaminiana bila ya woga vitisho au hofu kutoka kwa watu ambao wataguswa na utendaji wenu. Ili muweze kutekeleza majukumu yenu vyema hapa leo nataka nikukabidhini kitendea kazi yaani sharia ya reli No.10 ya mwaka 2017.

Ndugu Mwenyekiti, Ndugu Wajumbe na wageni waalikwa;

Baada ya kusema hayo naomba niwashukuruni tena kwa kunisikiliza na ni imani yangu kwa mara nyingine kwamba sio tu mmenisikiliza lakini

mmeyaelewa niliyoyaeleza na mtakua tayari kuyafanyia kazi. Na sasa natamka kwamba **BODI YA WAKURUGENZI YA SHIRIKA LA RELI NCHINI IMEZINDULIWA RASMI.**

Nawataakia utekelezaji mwema wa kazi zenu.

Asanteni kwa Kunisikiliza.